

**Dondoo za Mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam  
22 Machi 2008**

**Mahudhurio**

Ally Saidi Mwishehe  
Ally Salum  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Frank Peter Rwechungura  
Juma Ali Salehe Jongo  
Jumanne Idd Selemani  
Kassim Bakari  
Kibwana Mohammad Msiga  
Paulo Atibu Hatibu  
Sudi Saidi Ramadhan

**Barabara ya Morogoro**

Tulisoma pamoja barua tuliyopokea kutoka Halmashauri ya Jiji siku ya mkutano na Mama Mlamba. Haitoi majibu maalum ya maswali yote yetu, lakini inasema tutaalikwa kwenye mazumgunzo na semina. Elaine alitumia nakala ya barua yetu na maoni yetu kuhusu barabara ya Morogoro kwa email kwa AALOCOM na ITDP ili kupata majibu maalum.

Tulisoma pamoja mswadajari ya barua kwenda TANROADS Dar es Salaam kuhusu vifuniko vya mifereji maeneo ya Jangwani barabara ya Morogoro Road na Jumanne alisahihisha. Elaine ataweka sahihi na Juma ataipeleka.

**Ofisi, guta na mambo ya hela**

Ally Saidi Mwishehe alileta hela ya guta na Juma anayo hiyo hela – sasa ana Tsh 25,000.

Juma hajawahi kununua kamba kwa ajili ya rafu – atafanya wiki hii.

Sosthenes alipaka rangi kuficha alama ya msalaba na msikiti kwenye nembo ofisini wakati wa wiki kama tulivyokubali wiki jana.

Ally Saidi Mohammed alisema atakutana na Juma leo kwenda pamoja kupata bao la tangazo lakini hakuwepo kwenye mkutano.

**SUMATRA na matatizo ya usafiri ya wanafunzi**

Elaine aliongea na simu na David Mziray kumwuliza kama ameona barua yetu ambayo Juma alipeleka ofisini kwake lakini alisema hajawahi kuiona. Alisema anasoma email yake basi Elaine alitumia tena kwa email.

**Wamba Memorial Fund**

Bado hatujapata jibu la email wala voicemail message zetu kutoka Wamba memorial fund.

**Baisikeli za gurudumu tatu Ulaya**

Elaine alipata taarifa na picha ya matumizi ya baisikeli za gurudumu tatu Ulaya kutoka Robert Bartlett lakini alisahau kuja nayo ofisini – atakuja nayo wiki ijayo.

**Ufunguzi rasmi wa ofisi**

Tulibadalisha mawazo kuhusu ufunguzi rasmi wa ofisi. Tutahitaji viti, hema ya kulinda jua na mvua nje ya ofisi na kibali cha kutumia barabara. Wanachama walisema watafanya utafiti wiki hii kuhusu mahitaji haya. Tulikubali kuwaalika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, Halmashauri la Jiji Dar es Salaam na Mama Mlamba, TANROADS, wawakilishi wa manispaa za Ilala, Kinondoni na Temeke, Bwana Lupilya diwani wa Halmashauri ya Ilala, meya wa Ilala, AALOCOM, HUWATA, CHABADA, kampuni ya guta (Bwana Ngaja), na viongozi wa mtaa na kata wa Jitegemee.